**MUHTASARI WA RIPOTI YA UCHUNGUZI**
**MALALAMIKO JUU YA DHAMANA YA MIGA**
**YA MACHIMBO YA DHAHABU BULYANHULU, TANZANIA**

## 1. Utangulizi

Muhtasari wa ripoti ya uchunguzi hushughulikia malalamiko yaliyosajiliwa na Ofisi ya Mshauri wa Uchunguzi/Mikataba juu ya dhamana ya MIGA ya machimbo ya dhahabu ya Bulyanhulu karibu na Kahama, Tanzania.

Malalamiko yalisajiliwa na Lawyers Environmental Action Team (LEAT) kwa niaba ya Small Scale Miners of Kakola, Tanzania.

Muhtasari wa ripoti ya uchunguzi wakati uleule ulitolewa kwa pande zote za malalamiko. Hili ni jambo jipya katika namna ya taratibu za CAO, lakini ilikuwa kuhakikisha kuwa uchunguzi unapatikana kwenye pande zote zinazohusika, na kuhakikisha kuwa kadri inavyowezekana uchunguzi unaweza kusaidia pande zote husika kusonga mbele na kutatua tatizo kadri inavyowezekana na inavyohitajika. Kutokana na siri ya idadi ya watu waliotoa habari na uthibitisho, andiko hili ni muhtasari wa habari ya uchunguzi uliofanyika na CAO. Andiko linaeleza matokeo ya CAO katika mambo nyeti yaliyojitokeza katika malalamiko. Malalamiko ya awali yameambatanishwa katika kiambatanishi kwenye muhtasari huu. Ripoti imetolewa kwenye milki ya serikali na mlalamikaji.

## 2. Mradi

Bulyanhulu ni machimbo ya madini ya dhahabu yaliyopo kama kilometa 125 kusini magharibi mwa jiji la pili Tanzania, Mwanza. Eneo hili limeitwa jina kutokana na mto Bulyanhulu. Rasilimali yenye eneo la kilometa 54 mche mraba zimemilikiwa na watu wengi kwa kipindi cha miaka kumi. Eneo ambalo rasilimali hii hupatikana ni eneo ambalo kwa muda mrefu wachimbaji wadogowadogo wa madini wamekuwa wakishughulika.

Maji ya kusafishia mbale yamekuwa yakitolewa na Smith Sound kupitia bomba aridhini lililotoa maji kutoka Ziwa Victoria. Udongo huwekwa maji tena na kupelekwa kama lahamu kujaza shimo tupu chini ya ardhi au kwenye machimbo ya mabwawa. Shughuli ya ukandamizaji imepunguza kabisa kiwango cha maji kinachotumika katika machimbo ya madini na idadi ya udongo unaozalishwa.

Mwaka 1994, Serikali ya Tanzania ilitoa kibali cha uchimbaji madini kwa Kahama Mining Corporation Limited (KHMC), kampuni tanzu ya Sutton Resources. Juni 1999, Barrick Gold ilijipatia raslimali hiyo kwa kuinunua Sutton Resources.

Julai 1995, Serikali ya Tanzania ilitamka kuwa wachimbaji wote wadogo wadogo wa madini lazima waondoke eneo hilo, lakini hapakuwa na hatua yoyote ya kuhakikisha kuwa eneo hilo la ardhi limeamwa. Tamko hilo la Serikali ya Tanzania lilipingwa kotini na SSMC. Julai 30, 1996, Serikali ya Tanzania ilitangaza utaratibu wa kusafisha, na kutoa tamko la mwisho kuwa "wachimbaji madini wasio halali lazima waondolewe." Tamko lilipingwa na SSMC na amri ya kukataza ilitolewa tarehe 31 Julai. Haya yalibadilishwa 2 Agosti, 1996 na utaratibu uliendelea. Jambo hili lilitekelezwa Agosti 1996.

Mwaka 1998, Sutton Resources iliwaomba IFC kuwafadhili. Septemba 1998, IFC ilituma kwenye eneo hilo tume ya tathimini ya mazingira na jamii. Ombi la Barrick la kupata raslimali liliishia wakati IFC ilipojiingiza kikamilifu kwenye mradi. Hata hivyo, mwaka 1999 Barrick aliwaomba MIGA bima ya kinga ya kisiasa. Dhamana iliwekwa kwenye Bodi Desemba 21/1999.

**3. Malalamiko**

LEAT, kwa niaba ya Small Scale Miners Committee, ilisajili malalamiko mengi zikiwepo na barua ya malalamiko na pamoja na nyaraka za ushahidi. Mlalamikaji aliiruhusu CAO kutoa barua kwa MIGA, lakini sio kwa Barrick. Baadaye, LEAT ilifanya malalamiko kuwa barua ya wazi (kiambatanisho1).

CAO ilipendekeza kwa mlalamikaji kwamba, kwa kuwa hakuna lolote linaloonyesha siri ya mtu binafsi kwenye nyaraka za ushahidi, ni vyema kutoa nyaraka za ushahidi kwa walalamikaji wengine ili waridhike kuwa zinachukuliwa hatua za kutosha kushughulikia jambo muhimu. CAO walisubiri maelekezo kutoka kwa mlalamikaji kama watoe au wasitoe nyaraka za ushahidi. MIGA pamoja na Barrick Gold waliomba kuwa kama wanaweza kuziona nyaraka za ushahidi kusudi wajibu moja kwa moja kwenye tatizo.

Watu binafsi katika LEAT walikuwa wameshitakiwa na serikali ya Tanzania kwa kosa la uchochezi. Baada ya kusoma mashitaka, CAO iliona kuwa mashitaka hayo wala hayawahusu LEAT kama mlalamikaji kwenye ofisi hiyo. Pasipokuzungumzia maeneo maalumu ya mashtaka hayo, au utaratibu kisheria uliotarajiwa Tanzania, CAO iliamuru pande zote kutoa hadharani kila aina ya habari ambayo ingeliweza kutoa mwanga kuhusu tukio la Julai – Agosti 1996; hii ingeliwezekana kutoa mvutano juu ya malalamiko kwenye kiini cha mlalamikaji, kusudi watu wa Kakola na eneo lililozunguka wanaweza kuishi katika amani.

Kama Mshauri wa Uchunguzi/Mkataba wa IFC/MIGA, msingi wa uchunguzi huu uliangalia jambo kama linavyohusishwa kwa MIGA katika kujihusisha kwenye migodi ya madini. Kutokana na kwamba kabla ya matukio kulikuwapo na masuala yaliyohusu muda wa uchunguzi yakini, ili kuendelea na dhamana, ulipaswa kufikiliwa hapa. Hata hivyo, uchunguzi wa CAO ni ule wa kuhusiana na mlalamikaji. CAO haikushughulikia lalamiko yote kamili, wala haikujiingiza kwenye mbinu za uchunguzi wa haki na binadamu ambazo zingelijaribu kuhakiki au kutohakiki malalamiko mengi yaliyorudiwa na mlalamikaji, kwa mfano uchimbaji wa mashimo ya migodi iliyofungwa. Mojawapo ya madai ya walalamikaji ni kwamba uchunguzi huru na wenye haki ufanyike kuhusiana na matukio ya Julai – Agosti1996.

Mlalamikaji hugusia matukio kuhusu kuondolewa wachimbaji wadogowadogo wa migodi kutoka milki hapo Julai 1996; utoaji wa milki kwa Barrick Gold kutokana na ombi lao la Sutton Resources; uhamisho wa watu baadaye mwaka 1998; dhamana ya MIGA mwaka 1999; na madai ya shughuli ambazo zingelifikiliwa kinyume cha sera za juu ya mazingira na jamii za MIGA, ambayo ni sehemu ya Kundi la Benki ya Dunia.

Uchunguzi hugawa malalamiko katika vipindi vitatu:

- Matukio ya kwanza kabla na wakati wa mwaka 1996,
- Uhamisho wa watu mwaka1998, na
- Kuhusu uchunguzi yakini wa MIGA kama ilivyotayarishwa kwa ajili ya dhamana ya mwaka 1999, na shughuli za sasa za mgodi.

Matukio kabla na kwenye mwaka 1996 kwenye malalamiko ni pamoja na: kushindwa kupata kibali kinachostahili; namna ya usafishaji wa ardhi ulivyofanyika Julai – Agosti 1996; hati za kisheria za kumfukuza mpangaji katika harakati za usafishaji; jinsi waendeshaji walivyotekeleza au kutotekeleza sheria ya Tanzania na hukumu ya koti kuhusu usafishaji wa ardhi; ukosekanifu wa EIA kabla ya kuingia kwenye na ombi la kupewa eneo la Bulyanhulu; mipango ya maendeleo ya jamii na ile ya EIA ambayo ilitolewa kwa Serikali ya Tanzania na MIGA haikuonyesha njia ya mabadiliko ambayo yanaweza kutokeza athari katika mali ghafi, kulazimishwa kuondoka kwa walalamikaji wakati wafadhili wa mradi walipolichukua eneo la mradi; Serikali ya Tanzania na wafadhili wa mradi walishindwa kugharimia au kuweka mpango wa makazi; na Serikali ya Tanzania na wafadhili hawakufidia uharibifu wa mali na maisha.

Malalamiko juu ya matukio ya 1998 yanayo madai yaleyale sawa na yaliyotajwa hapo juu kuhusu namna ya mashauriano, utaratibu wa kufukuzwa na kusafisha ardhi, makazi na fidia.

Malalamiko kuhusu shughuli za MIGA ni pamoja na madai kwamba MIGA ilishindwa kufanya uchunguzi makini wa kina na ustadi kuhusu taarifa juu ya kipato cha ufadhili wa mradi, umilikaji na uendeshaji wa Bulyanhulu kuimarisha ukweli wa taarifa zilizotolewa na usahihi wa maoni yaliyotolewa na wafadhili wa mradi kabla ya kufanya maamuzi kutoa dhamani ya bima kisiasa; na kuwa MIGA ilishindwa kuandaa/au kuweka wazi kwa walalamikaji na pande zote taarifa nzima kuhusu habari na hali halisi juu ya kipato cha wafadhili wa mradi, umilikaji na uendeshaji wa mradi, mbali na walidaiwa kufanya hivyo mara nyingi.

Malalamiko kuhusiana na hali ya sasa ya uendeshaji ni pamoja na madai kwamba kuna matumizi ya nguvu, au pamoja na vitisho vya utumiaji wa nguvu kuwafukuza watu kutoka eneo la mgodi, kuwaingilia watu katika eneo la kuishi kwa amani na kufurahia haki yao ya umilikaji, kuzuia kutumia ardhi kwa kilimo na kusimamisha ujenzi wa nyumba; utaifishaji wa ardhi kumesababisha kuanguka kwa uchumi katika eneo la Bulyanhulu, hasa Kakola; kwamba kuna mbinu wazi za kudhoofisha matumizi ya Kakola kama senta ya wananchi na biashara; kwamba zitatokeza athari kubwa kwenye jamii zinazozunguka; na kwamba kuna kushindwa kubuni nafasi za ajila kwa wenyeji wa pale.

Mbali na mafungu haya matatu ya maswala ya madai kati ya walalamikaji, walalamikaji hupinga urazini wa Kundi la Benki ya Dunia kusaidia moja kwa moja vitega uchumi vya kigeni katika Tanzania.

## 4. Matukio ya Julai 1996

Mlalamikaji hurudia madai yake dhidi ya viongozi wa serikali na mgodi, kuhusiana na matukio mwishoni mwa Julai na mwanzoni mwa Agosti 1996 ambayo hujumuisha vitendo viovu na vya uaji. Madai haya ni ya kudumu na yamekuwa vikirudia na vyombo vya habari na mashirika ya kimataifa na yasiyo ya kiserikali.

CAO haina mamlaka au uwezo kuchunguza madai dhidi ya Serikali ya Tanzania. Matukio ya 1996 yalitokea wakati Kundi la Benki ya Dunia halina madai katika uendeshaji na zaidi ya miaka mitatu kabla MIGA haijatoa dhamana. Hata hivyo, kadri ya madai yalivyotolewa, kuna angalau kuhatarisha sifa kwa MIGA katika uamzi wake wa kutoa dhamana, CAO ilipenda kuonyesha shughuli za MIGA na za mteja wa MIGA, Barrick Gold, kujiridhisha sawa na msingi wa madai kuhusu walivyoendesha uchunguzi wao yakini.

Madai yalitolewa na kurudiwa na LEAT katika malalamiko yake kwa CAO sio mapya. Hata hivyo, LEAT husema kwamba inao ushahidi mpya, yaani video ambayo huonyesha kumbukumbu za sasa za miili ikifukuliwa kwenye mashimo ya wachimbaji wadogowadogo wa migodi. Mashimo haya yanadaiwa kuwa yaliunganishwa na kufukiwa kama matokeo ya kufunga ardhi iliyofanywa na wamilikaji, Sutton Resources, katika kipindi cha mwezi mmoja kilichofuata Julai 30,1996 baada ya Serikali ya Tanzania kutangaza kwamba ardhi lazima iamwe.

CAO haiwezi kuwa na uhakika kuwa video huonyesha lile ambalo LEAT inapenda kulionyesha. Nafasi, tarehe, muda na yaliyomo hayawezi kudhibitishwa. Kwa hiyo, siyo wazi kwamba video huonyesha wachimbaji wadogowadogo walionyongwa kama matokeo ya kusafisha ardhi katika tarehe zilizofuata Julai 30, siku ya tangazo. Zaidi ya hapo, CAO ilipata mashahidi na kumbukumbu za karibu ambazo zingelipinga ushahidi wa matukio ambayo LEAT hudai unaelezwa na video. Wakati wa tume kwenye eneo la utafiti la Bulyanhulu  wachimbaji wadogo wa migodi, kuna waliielezea tume ya CAO wale ambao walijua pale video vilipopaonyesha kwa uhakika na mahali ambapo matukio yalichukuliwa, kisha waliipeleka tume ya CAO mahali hapo. Hata hivyo, hawakuwa na uhakika kwamba wachimbaji walionyeshwa wakiburutwa kutoka kwenye migodi ya madini na wakiuawa kama matokeo ya usafishaji ardhi, hivyo hawakuweza kukubaliana na ushahidi wa matukio LEAT waliodai kuwa video iliyaonyesha.

LEAT hudai kuwa wachimbaji wadogowadogo wa migodi wana haki ya kumiliki raslimali za madini katika eneo la madini la Bulyanhulu, na kuwa raslimali hizi ziliahidiwa kwa Small Scale Miners Committee na mfuatano wa wanasiasa katika Tanzania miaka na miaka.

Ni wazi sasa kwa CAO kwamba eneo la mradi (milki) liliahidiwa kwa watu mbalimbali kwa wakati tofauti ikiwemo Small Scales Miners Committee na kampuni za migodi. Hata hivyo, pamekuwapo na taratibu za sheria katika Tanzania juu ya umilikaji wa Sutton Ressources na haki ya milki ya wachimbaji wadogo wa madini. Utaratibu huu ulijulikana sana katika eneo hili. Inaonekana wazi kuwa tangazo lilipotolewa na viongozi wa serikali pale Kakola Julai 30 kuwa eneo milki liachwe wazi na wachimbaji wa madini wasioruhusiwa kisheria wafukuzwe, wachimbaji wadogowadogo wa madini walikuwa wamefanya hivyo tayari. Pengine, wachimbaji

wa madini walifahamu lile ambalo lingetokea, na waliendelea mbele kwenye maeneo ambapo wachimbaji wadogo wa madini walipokuwa.

Nyongeza ya mashitaka ya haki ya Sutton Resources kuchimba madini kwenye milki, LEAT hudai kuwa utaratibu ambamo ardhi ilisafishwa hapo Julai 30 na siku zilizofuata ilitokeza watu 52 wasiojulikana majina yao kuzikwa wakiwa hai kwenye shimo walimokuwa wakifanyia kazi. Pia ilidai kwamba katika utaratibu uliotumika kusafisha ardhi ulifanya watu kati ya 70,000-600,000 kufukuzwa kwenye ardhi katika kipindi cha siku hizo.

Wakati eneo hili ni kati ya migodi midogo kihistoria, idadi ya wachimbaji na jamaa zao huishi katika eneo hili huzidi kuongezeka kila mara. Katika machimbo ya dhahabu mapema miaka ya 1990, kuna hesabu ya mamia elfu ya watu wanaoishi katika eneo hilo. Mashirika ya misaada na maendeleo huhesabu mia elfu ya watu mwanzoni mwa mwaka 1990. Kadri wachimbaji walivyomaliza tabaka za dhahabu ambayo inaweza kufikiwa na wachimbaji wadogowadogo wa madini – hadi meta 10 chini ya ardhi – wachimbaji na jamaa zao waliondoka. Walipoingiza vifaa vya bomba la maji katika eneo hilo, uchimbaji uliongezeka kwa maana shimo lingeingia ndani kama meta 60. Hata hivyo, kama matokeo ya vifaa vya uchimbaji na ujuzi ambao eneo hili lilizuiwa kwa ajili Kahama Mining Corporation, na kwamba wachimbaji wadogowalikuwa wameama nje ya ardhi hiyo, labda palikuwepo na maelfu ya watu wachache katika eneo hilo wakati uamuzi wa kuanza kusafisha ardhi hiyo ulipofanyika mnamo Julai 30. Wachimbaji husema kuwa labda palikuwepo maelfu kadhaa. Kwenye ripoti ya Amnesty International katika Serikali ya Tanzania juu ya Bulyanhulu, husema labda watu 2,000 waliathiriwa na tamko lilitoa amri ya kufukuzwa. Kwa hiyo, CAO hujumlisha kuwa watu kadha walikuwa wakifanya kazi Bulyanhulu Julai 29 na kwamba na walienda kwenye migodi mingine baada upakizi wa magogo yao ya mbao, mabomba na vifaa vingine kwenye roli. CAO inao uhakika kuwa idadi ya watu ni kati ya 200 – 2,000.

Kwa kiasi kipi kulikuwepo na shughuli katika mashimo wakati wa kiangazi cha 1996 kunaweza kuthibitishwa na picha toka angani ambayo inaweza kuonyesha mashimo mengi yaliyofukiwa na kuachwa wazi. Hakuna alama kutoka picha za sasa kwamba kuna mamia au makumi elfu ya watu kwenye ardhi hiyo kwa sasa. Hii pengine inaweza kuthibitishwa na picha za setelaiti kama zingelikuwepo katika eneo hilo kwa wakati huo.

Kamati ya wachimbaji migodi wadogo walitoa kwa CAO orodha ya wamilikaji wa mashimo na ilieleza kuwa kila shimo liliajili watu 70 na jamaa zao; hivyo karibu ya watu 30 walikadiriwa kuwa kila shimo. Hata hivyo, orodha ya wamilikaji haikuwa na tarehe; na kama inavyoonyesha hapa juu, wakati uleule, mashimo mengi yanaonekana kutokutumika. Kamati yenyewe ilikubali kuwa siyo mashimo yote yaliyoorodheshwa ambayo yalikuwa yakitumika wakati wa usafishaji wa ardhi. Zaidi ya hapo, data za uchunguzi za Sutton Resources na makadirio ya viongozi wa Tanzania kule Kahama huonekana kuonyesha kuwa kulikuwepo na watu wachache zaidi kuliko mamia elfu yaliyotajwa kwenye malalamiko. Wenyeji wa Kakola pia walidhibitisha kuwa watu wengi waliondoka kabla ardhi haijasafishwa mnamo Agosti 1996.

Mchezo wa idadi umekuwa wa kuvutia katika habari ya madai ya Bulyanhulu. Idadi kutoka utafiti wa eneo zimepambwa na kutiwa chumvi miaka na miaka. Wafanyakazi wa Sutton Resources wanazo picha zinazoonyesha wachimbaji wadogo wa migodi walio salia wakiondoka

eneo la Bulyanhulu kutokana na tangazo la Julai 30. Sura iliyoonyeshwa na walalamikaji kuhusu kuondolewa kwa watu mamia elfu, kama siyo makumi elfu, katika msafara, kwa siku chache tu, kulivuta serikali kuu na mashirika ya kimataifa katika eneo hilo. Hata hivyo, hakuna anayeweza kuthibitisha kuhamishwa kwa kiasi kikubwa nchini. Ingelikuwa inafanana na kuamishwa kwa wakimbizi katika maziwa makubwa mwaka mmoja au miwili kabla.

Katika Julai 30, 1996, kutokana na kupinga madai ya kesi mahakamani, Waziri wa Madini na Nishati wa Serikali ya Tanzania aliamrisha kwamba wachimbaji wote wasio halali katika raslimali ya Bulyanhulu lazima wasimame kuchimba kufikia mawio ya jua ya asubuhi iliyofuatwa (Julai 31), kwamba waondoe nyenzo za kazi za uchimbaji kufikia Agosti 7 na kwamba kufikia Agosti 30 lazima wawe wameihama raslimali hiyo. CAO haina ruhusa kuhoji ukweli wa tamko hili.

Tamko lilitolewa na viongozi wa serikali kwenye mji wa Kakola na sehemu zote za eneo hilo kusudi kuhakikisha kuwa watu wanajua juu ya uamuzi huo. Watu hutoa taarifa kuwa walijua kutokana na habari katika matangazo ya redio. Tamko hili, lililodhibitishwa kwa kina chake na watu wengi katika Kakola, halitaji kuwa mashimo yaliunganishwa na kujazwa Julai 31 au Agosti 1, 1996. Nyaraka kutoka kwenye machimbo ya madini huonyesha kwamba uunganishaji na ufukiaji kwenye machimbo ya madini haukuanza mpaka ardhi ilipokuwa – Agosti 7. Risiti za waliofanya kazi ya kusomba wakati wa kusawazisha kusafisha kuonyesha idadi ya mashimo yaliyojazwa kila siku. Imedaiwa na LEAT na washiriki wake wa kimataifa kuwa upotevu wa kila waraka kutoka machimbo huonyesha kuwa kila taarifa imepotea au kuharibiwa. Inadaiwa kuwa machimbo yalijazwa mara moja baada ya tamko, na kuwa shughuli ilifanyika kwa haraka, watu walitekewa ardhini kwa maana hawakuwa na muda wa kutosha kuondoka.

CAO, baada ya kuchunguza ushahidi wa SSMC, LEAT, kuzungumza na wenyeji, wafanyakazi wa mgodi, watu walioshuhudia, kuangalia ripoti za polisi na kuchunguza waraka uliotolewa na Barrick Gold, imefikia patano kuwa ujazaji wa machimbo ya mgodi ulifanyika siku kadhaa baada ya tamko, kuwa ilikuwa kazi ya kujitolea na kuwa mtu mmoja alitumika kusomba udongo. Kwa hiyo, shughuli ilikuwa ya haraka sawa na nguvu ya msombaji udongo wa mtu mmoja ilivyoruhusu. Hakuna ushahidi tosha kuthibitisha matamko ya baadhi ya wanachama wa SSMC kuhusiana na namna mashimo yalivyojazwa. Hata hivyo, kuna ushahidi ushuhuda nyingi katika eneo hilo kupinga madai ya SSMC.

Uchimbaji mdogo wa migodi ni kazi ya hatari duniani. Mpaka ardhi ilipoachwa wazi, hakuna mashaka kuwa wachimbaji madini wengi walikufa miaka na miaka kutokana na moshi au machimbo kuporomoka. Walalamikaji hawakatai hili na wanakumbuka kuwa mara nyingi waliwaambia viongozi juu ya uporomokaji au vifo. Kwa sehemu nyingi miili ya hao waliouawa haikuweza kuonekana.

Utaratibu wa uchimbaji mdogo wa mgodi ulikuwa kwamba mwenye shimo alilipia maji ya bomba aliyotumia ( baada ya bomba kuingizwa katika eneo hilo mwaka 1995) na kisha alipashwa 20% ya mapato SSMC, ambayo iligawanya pesa kwenye wodi. Maoni jinsi shughuli za SSMC zilivyoanza ilikuwa tofauti. Baadhi ya wanachama wa SSMC, ambao wamejiingiza kupinga dhidi ya mgodi na wako mstari wa mbele kudai fidia kwa kupoteza mapato, kupoteza nafasi ya kutumia raslimali kwa kuvurugwa, SSMC ilifanya kazi kama muungano [wa chama]

ingawa isiyo na haki ya kuweka utaratibu katika eneo hilo. Kwa wengine, SSMC iliundwa kwa ujanja kwa kutumia mbinu za vitisho ili kujipatia mapato kutoka kwa wamilikaji mashimo. CAO ilisikiliza namna zote kutoka kwa wenyeji kutoka katika eneo hilo. Idadi ya dhahabu iliyouzwa kwa magendo katika nchi ya jirani ya Kenya haiwezi kuchunguzwa kwa uhakika na CAO, lakini inaonekana kuwa ilikuwa idadi kubwa. Kwamba SSMC ilijua hili, kama siyo yenyewe ndiyo iliyohusika, inaonekana kuwa hakuna mashaka katika hilo. Hili ni jambo nyeti katika uamuzi baadaye kwa madai kwamba wachimbaji "wanaiba" uchumi wa Tanzania kwa njia ya moja kwa moja ya wawekezaji wa nje.

Picha iliyopatikana kutokana na mahojiano na uongozi wa SSMC pamoja na wenyeji pamoja na wachimbaji mgodi na watenda kazi mahali hapo mwaka 1996 na kabla, ni kuwa SSMC ilikuwa imeratibishwa vizuri hasa – jibu lao katika mwaka 1996 kutafuta kibari kisheria kuzuia amri ya kusafisha ardhi hiyo - inaonyesha dalili hizo. Taarifa haikutegemewa. Hii ilitokea ghafla kwa njia ya ghasia ambazo zilitokana na tamko la mwisho la kuondoka katika ardhi, lilivyotolewa Julai 30.

Suala la kulipwa fidia kwa wachimbaji wadogo wa migodi wakati wa amri ya kuondoka kwenye ardhi mwaka 1996 ni kati ya Serikali ya Tanzania na wachimbaji wadogo wa migodi na linaangukia kwenye mahakama kuu ya serikali ya Tanzania. Kwa wakati huo mgodi haukuwa mradi wa Kundi la Benki ya Dunia na kwa kuwa tendo la kusaidia makazi lilikuwa la hiari, hakuna mwongozo wowote wa Benki ya Dunia ungeamriwa kutumika.

Mlalamikaji hudai kuwa kama watu 52 waliuawa wakati wa harakati za kusafisha ardhi, walinaswa hai kwenye mashimo na wachimbaji migodi na wafanyakazi wa serikali ya kijiji kutokana kuunganisha na kufunika mashimo ya migodi. Haya ni madai juu ya mauaji yaliyokusudiwa. Hayawezi kuwa madai makali zaidi. CAO imeomba orodha ya majina ya watu 52 ambao waliuawa kwenye siku za kwanza Agosti 1996 kama zilivyoelezwa na mlalamikaji. Amnesty International imetambua kuwa ushahidi wa vifo vya watu 52 unatokana na habari iliyotolewa na SSMC ambao sasa hawapo katika eneo hili kwa sasa. Sasa wanapendekeza kuwa orodha ya majina ya wale waliouawa ni lazima yawekwe mwanzoni ili kuanza uchunguzi muafaka nchini Tanzania. CAO imeacha kuchunguza hilo kutokana na kwamba orodha haikuweza kutolewa na wenyeji, serikali ya kijiji, au SSMC aliye mlalamikaji katika kesi hii, hii hutokeza mashaka juu ya ukweli wa madai kwamba watu hawa walifariki katika harakati za kuziba machimbo ya migodi mapema Agosti 1996.

Tume ya CAO iliyokutana na wenyeji waliosema kuwa jamaa zao ni kati ya 52 waliofariki. Hata hivyo majirani walichukua tahadhari kuiambia tume ya CAO kuwa jamaa hao bado wanaishi na ni wazima au kwa namna moja walikufa kwenye hajali ya machimbo kabla ya Agosti 1996. Kwa upande mwingine, vyombo vya habari vya Tanzania vimegundua kuwa watu hao wanaishi katika sehemu nyingine za nchi, ambao walidaiwa kuwa wamekufa kwa muda huo.

Malalamiko na mashirika ya kigeni wameomba kama pangelikuwepo uchunguzi wa kujitegemea juu ya matukio haya kugundua kama palikuwepo mauaji yaliyotokea au ukiukaji wa haki za binadamu zilizotokea. Serikali ya Tanzania kwa matukio mbalimbali imeonyesha wazi kuwa hakuna kesi ya jinsi hiyo yenye kuhitaji uchunguzi wa aina hiyo.

Mlalamikaji ameomba madai kama hayo husikilizwa kutokana kwamba video ilitoa uthibitisho muhimu. CAO, pasipokuwa na orodha ya watuhumiwa, ingawa video inaweza kuonyesha yale yanayodaiwa kutokea, kuna utata mwingi wa ushahidi kuhusu yaliyotokea katika siku hiyo kutoka kwa watu wenyewe, hivyo haionekani CAO kupendekeza huchunguzi huru. Uamuzi umebakia mikononi mwa Serikali ya Tanzania.

Amnesty International imekuwa mstari wa mbele kudai uchunguzi huru. Hata hivyo, CAO imegundua kuwa Amnesty International haijakuwa na uchunguzi juu ya madai yenyewe wala haijawahi kuwa katika eneo hilo au kukutana na wenyeji, walioshuhudia au wengineo, [Amnesty International] imekaa mbali na chanzo cha madai kulingana na  Ripoti ya Mwaka 1997. Sasa inarudia madai kama madai na kudai uchunguzi huru ili kugundua ukweli. CAO baada ya kuchunguza nyaraka zinazopatikana haijaona kuna haja ya lazima ya uchunguzi.

**5. Matukio ya 1998**

Mwaka 1998, mzunguko wa kupata makazi yalifanyika na IFC iliyataja hapo nyuma kwenye ripoti yake ya kiofisi, iliyoandaliwa na tume iliyotumwa kufanya ziara ya tathimini ya hawali. Makazi  mfano wa yale ya 1996, hayakufanyika kadri ya sera ya Kundi la Benki ya Dunia juu ya makazi yasiyotegemewa; wakati huo Benki ya Dunia haikuwa na maslahi yoyote kwenye mradi. Haiwi wazi kiasi cha kuonyesha tatizo lililopita juu ya makazi mapya yaliyofikiriwa na MIGA na mwongozo ulitolewa jinsi ya kurudia upya makazi au vipengele vya shughuli ya makazi yasiyo kusudiwa vilivyoelezwa na wafadhili wa mradi wakati wa dhamana. MIGA ilipendekeza kuwa wafadhili wa mradi wawatunze wale watu waliohamishwa kuhakikisha hakuna hali mbaya zaidi baada ya makazi mapya, hata kama makazi mapya yalifanyika kabla ya MIGA haijajiingiza. Lakini jambo halikuwa hivyo, na wachimbaji migodi hawakuelewa kwa utondoti juu ya sera ya makazi yasiyokusudiwa kama ilivyotekelezwa na IFC wakati tume ya CAO ilipokuwa kwenye mgodi.

CAO waligundua kuwa jamaa wale waliamishwa mwaka 1998 walikuwa wakiishi kwenye hali ya umaskini nje ya mgodi lakini pia kwenye milki. Walisema ijapokuwa wanaishi kwenye eneo milki hawakuwa na uhakika wa jambo la kufanya au la kutofanya katika ardhi hiyo. LEAT ilisema kuwa wenye mgodi walikataa kuwaruhusu watu kupanda mazao na kwa hiyo watu hao wakapatwa umaskini mkubwa. CAO haikupata ushahidi wa sera ya pamoja au katazo la wenye madini kuwa watu walioishi kwenye milki wasipande mazao, bali CAO iligundua kuwa hapakuwepo na usalama katika jamaa hizo kwa kuwa walitegemea kuamishwa tena karibuni kwa hiyo walipunguza kulima na kupanda. Palikuwepo na uwezekano wa mawasiliano ya hali ya juu kati ya wenye mgodi na familia ambazo zilikuwa zinaishi kwenye milki, pia ilikuwa wazi juu ya yale watakayofanya na wasiyotakiwa kufanya katika ardhi hiyo hata pia kuhusu hali yao ya baadaye. CAO iliamsha masuala haya wakati uleule wa tume kwenye mgodi. Hii ni aina ya masuala ambayo CAO ilitegemea kwa kweli MIGA kuchagua katika uangalizi wake wa kundi A la dhamana, lakini MIGA haikufanya hilo.

**6. Shughuli za uchunguzi yakini za MIGA**

Septemba 1998 tume ya tathimini ya mazingira na jamii kutoka IFC ilikwenda Bulyanhulu kama itikio la ombi la Sutton Resources kwa ajili ya masuala ya pesa ya IFC. Miradi ilikuwa imejulikana kama kundi A.Tume pia ilikuwa na wataalamu wa uwekezaji.

Enivironment Impact Assesment iliandaliwa kwa ajili ya migodi na Nerecol Dames & Moore kulingana na sheria za Serikali ya Tanzania. Tume ya IFC ilitarajia EIA kutii yale yaliyodaiwa na Serikali ya Tanzania. Hata hivyo, kutimiza madai ya Kundi la Benki ya Dunia katika uendeshaji kwa wakati huo na IFC, tume ya IFC iliona kuwa nyongeza ya mambo mengine ungeliitajika ili kuitikia masuala mengine ambayo yangelikuwa yaboreshwe. Tume ya IFC imegundua kabisa kwamba uboreshaji wa barabara haukuwa umeingizwa katika EIS; bomba la maji kutengenezwa kutoka Smith Sound kwenye mgodi lilikuwa jambo la kushughulikia, na suala la makazi na fidia kuhusiana na bomba la maji, eneo la bomba ya migawisho na mgodi vingelishughulikiwa; na kuwa EIS haikugusia masuala ya nyuma wakati wa usafishaji wa ardhi.

Tume ya IFC iligundua kwa utandoni mabaki ambayo yangelidai kufanya mradi ukubaliane na sera za IFC na kuzungumzia masuala ya sifa katika matukio yaliyodaiwa mwaka 1996. IFC ilipendekeza nyongeza kwa EIA kuandaa utondoti wa yale yatakayohitajika kuhusiana na mawazo yalivyoorodheshwa hapo juu.

Pamoja na kibali cha Sutton Ressorces kilichotolewa na Barrick, suala la IFC halikuwa tena muhimu. Julai 1999 Barrick aliomba MIGA bima. MIGA iliwaendea IFC kupata habari za msingi na iliambiwa kuwa IFC haikuwa tena inashughulika na mradi. CAO huelewa kuwa mazungumzo baina ya wafanyakazi husika wa MIGA na IFC hayakuwa rasmi na kuwa wafanyakazi wa MIGA walijua madhumuni ya ripoti ya IFC kwenye jumlisho ya tume yake ya uchunguzi. Hata hivyo, mbali na hii CAO haikuweza kupata mawasiliano yoyote kutoka MIGA kwenda Barrick Gold au mfanyakazi kutoka MIGA au Barrick kuyakinisha kuwa masuala yaliyoibuka nyuma ya ripoti ya ofisi yalishughulikiwa na MIGA. Ijapokuwa mradi unaweza umebadilika kutoka IFC – Sutton, MIGA - Barrick na kwamba Barrick inaweza kuwa imeshughulikia masuala mengi yaliyoorodheshwa kwenye ripoti ya nyuma ya ofisi kuhusu IFC / pakiwepo makazi mapya na matukio ya nyuma.

MIGA ilihakikisha kuwa CAO ilikuwa sawa na dhibitisho za Barrick katika masuala haya. CAO haina sababu ya kuweka Barrick katika jambo hili. Hata hivyo, katika suala fulani MIGA iliona au ilijisikia kutafuta udhibitisho huru wa masuala nyeti kutokana na ukweli wa kundi A la dhamana ya mradi. Shabaha na kusudi la haki ya uangalizi yakini kwamazingira na jamii katika Kundi la Benki ya Dunia ni kutoa kuwa uchunguzi huru na sahihi Kusudi kundi lisibaki “kuamini” tu wafadhili.

Mwisho, ripoti ya nyuma ya IFC haiwezi kufaa kuwa kama uchunguzi yakini na IFC imeweka wazi hali yake kwa MIGA. MIGA ilitamka kwa CAO kwamba iliweka msingi wa kazi kwa IFC, hata hivyo haionekani kushughulikia jambo kwa mtazamo wa IFC. CAO inapendekeza kuwa tendo la IFC kushughulikia uchunguzi yakini au matokeo ya kazi ya IFC ambayo hutumika kama wakili kwa uchunguzi yakini wa MIGA lazima yafanyike rasmi na kufahamika na pande zote.

**7. Hali ya sasa – madai ya unyanyasaji, kuingiliwa na kudharauliwa kwa jamii.**

CAO haikupata msingi wa madai ya sasa ya unyanyasaji, kuingiliwa au kudharauliwa kwa jamii na wenye mgodi. Kwa bayana, shughuli za maendeleo juu ya kitega uchumi cha aina hii na mwenendo katika eneo hili kuwa hudhoofisha hali nyingine za uchumi na huduma za jamii ni ngumu na hutoa changamoto kabisa. Hata wenye mgodi wameingia kwa kushirikiana na wananchi na washika dao wengine wa Mashirika yasiyo ya Serikali na Serikali katika mkoa.

Kakola, ambayo iko nje ya lango kuu la mgodi, ni jamii ambayo inateseka kutakana na mifumo ya jamii katika maeneo ya madini. Utajiri wa mji unabadilika kutoka nyakati za shughuli za wachimbaji wadogo wa mgodi, na mipango ya maendeleo na maono kwa ajili ya jamii lazima viwe vimebuniwa na viongozi wa jamii ile kwa ushirikiano na wenye mgodi na serikali za kijiji. Uzuiaji wa uenezaji wa UKIMWI na magonjwa mengine ya zinaa, na kushughulikia shida ziletwazo na ulevi na ghasia ni wajibu wa watu wote, lakini CAO iliona kuwa wenye mgodi walijua zaidi ya wajibu na kazi yake, na ilifikiri kwamba mipango yake na ushirikiano wengine ni muhimu. Changamoto kwa wote, hasa Kundi la Benki ya Dunia, ni namna ya kuhamasisha kitega uchumi cha Barrick katika eneo hilo ili kuwekeza katika nyanja nyingine za uchumi na maendeleo na huduma za jamii, katika kuboresha maisha ya watu katika eneo la mradi kwenye wilaya.

## 8. Jumlisho

CAO inahusika na taratibu rasmi zinazoendelea kati ya IFC na MIGA kuhusu Uchunguzi yakini. Ni wazi kwamba kama shirika dada kati ya Kundi la Benki ya Dunia, ushirikiano lazima uhimizwe. Hata hivyo, wakati IFC inapotoa ushauri na kuchukua wajibu wa MIGA wa uchunguzi yakini, lazima hayo yawe kwenye mkataba ambao hautadai uwajibikaji kama mapendekezo hayakutekelezwa.

CAO pia inaona kwamba MIGA haikuchunguza kwa kina mradi kutokana na ziara ya Awali ya tathimini. Uchambuzi wa nyaraka pasipokuwepo kwenye eneo la utafiti hakufai, hasa mabadiliko kwenye mradi, tofauti ya muda kati ya wachambuzi wa IFC. Katika hali hii, MIGA imekuwa ikiudumiwa vizuri na wenye mgodi na mfadhili wa mradi ambao walijitoa kwa huduma nzuri. Ni kwa sababu hii na siyo kwa sababu ya ukaguzi au uchunguzi yakini wa MIGA kwamba mwenye mgodi anatenda kwenye viwango vya mazingira na jamii ambavyo viko katika matarajio ya uwekezaji ya Kundi la Benki kuu.

Hadi leo, hakuna mtaalamu wa mazingira au jamii aliyekwisha kuizuru Bulyanhulu. Zaidi, katika mazungumzo na uongozi wa mgodi na wafanyakazi kulikuwepo na maelezo ya mambo waliyoyapendelea kama mifano ya utendaji bora katika maendeleo ya jamii, maeneo ambayo Kundi la Benki ya Dunia huwa mstari wa mbele. MIGA lazima ijue mamlaka na utayari wake kuwasaidia wateja wake katika kutoa na kuendeleza utendaji bora, na kutoa huduma kama chanzo cha habari na kusaidia wakati mteja anashindwa kufanya hivyo.

CAO haiamini kuwa mradi hutimiza masharti ya ukaguzi wa mahesabu na ilifurahishwa na namna mgodi ulivyoendeleza uwezo wa jamii na mazingira yake. Masuala ya uongozi na ugawaji wa mapato na tofauti kati ya kitega uchumi katika eneo la Bulyanhulu ambalo ni eneo maskini sana katika mikoa ya Tanzania, na jinsi faida tosha inavyowezakupatikana kwa ajili ya

wenyeji ni la kudumu kwa IFC na MIGA. Kadhalika inaonekana kuwepo nafasi zaidi ya mbinu hai zilizo ratibishwa katika suala kati ya MIGA na Benki ya Dunia na mawakala wengine hai katika Tanzania. Pasipo mwongozo kutoka MIGA, Barrick Gold imeanzisha uhusiano mzuri na taasisi za misaada za kimataifa na mashirika ya maendeleo kuboresha shughuli za maendeleo na [ jitihada] hizi lazima ziungwe mkono na matokeo yake ya maendeleo lazima yasimamiwe.

CAO haiamini kwamba inaweza kufanya wajibu zaidi bora katika suala hili. CAO kwa hisani huwaomba walalamikaji na washika dao wake wa kimataifa wachunguze namna wanavyotumia taarifa na mkazo wanaouweka katika udhibitisho. Kutetea wananchi ambao wanaweza kukosa namna ya kusikiwa na serikali na katika mamlaka ya kimataifa imekuwa mbinu iliyojaribiwa na kupimwa kuwa ni ya kulazimisha mabadiliko. Mashirika yasiyo ya kiserikali ya kimataifa katika eneo hili, makundi ya maendeleo na haki za binadamu wana kumbukumbu tosha za kusukuma Kundi la Benki ya Dunia kuwa na mbinu kabambe za makadirio ya mazingira na jamii kati ya jitihada nyingi za sera. Kadhalika, mashirika yasiyo ya kiserikali ya kutetea haki za binadamu hutekeleza wajibu maalumu katika kutenda kama dhamiri ya kiulimwengu na yametokeza mabadiliko katika mielekeo ya mashirika ya watu binafsi pakiwepo viwanda vya kusindika rasilimali. Lakini CAO huamini kuwa kuna kuwajibika kunakoendana na wajibu mpya.

Katika kutokeza madai ambayo hayawezi kudhibitishwa na madai yanayorudiwa ambayo mtu anajua kuwa siyo kweli yanaweza kudaiwa kuwa mbinu halali katika kampuni au mapambano. Hata hivyo, kuna gharama yake. Gharama yake ni kwamba ukweli, uzito wa hoja na hatimaye kujihusisha kisheria kwa mashirika yasiyo ya kiserikali katika kazi ya namna hiyo utapingwa. Hatari ni kwamba msukumo wa sasa wa sauti ya wananchi unapashwa kuwa na msingi. Hii ni vibaya kwa shughuli za sauti ya wananchi, ni vibaya kwa marekebisho ya Kundi la Benki ya Dunia ambalo watu wengi hulitafuta, na hatimaye ni vibaya kwa watu ambao kwao madai yanafanyika, kwa maana mwishowe wanachezewa na kunyamazishwa zaidi. Nani atakaye wasikiliza sasa?

Kurudia madai mtu anayojua si kweli, hasa madai ya mauaji, kuna matokeo yake. Kuna matokeo kwenye sifa ya biashara na uwezo wa biashara wa kampuni binafsi na kwa watu wanaohusika. Pia kunaweza kukawepo matokeo kisheria juu ya matendo kama hayo. CAO inasikitishwa na baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayofikilia kuwa wanaweza kuepuka adhabu katika jambo hili. Kwa kweli CAO huamini kuwa hakuna kukwepa adhabu. Matokeo yanaungwa mkono dhidi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yasiyowajibika. Hili ni eneo hatari kwa maana pande nyingi zipo tayari kupinga sauti ya wananchi ya jinsi katika shughuli za maendeleo.

Lawyers Environmental Action Team (LEAT) inayo historia nzuri kuleta hadharani sheria ya uma katika masuala ya mazingira katika Afrika Mashariki. Hata hivyo, katika jambo hili, CAO imeona kuwa LEAT imekuwa huru mno kwa kuchukua na kuchagua utaratibu wa maadili ambao kwao hiyo itayafanyia kazi. Kwanza, katika utaratibu wa mshauri wa mikataba, uhusiano baina ya Mshauri wa Mikataba na mlalamikaji ni wa fadhila, na unaweza kuwepo kwa imani. Wakati huohuo, CAO iliona kuwa imani hiyo haikuwepo na kuamua kuwa mlalamikaji mbele ya CAO alikuwa mmojawapo ya njia zilizotapakaa zikielezeka hasa kwenye utangazaji wa hali ya juu na watu binafsi ndani ya LEAT na ajenda zao za ndani. Makala kwenye vyombo vya habari visivyosubiri ambavyo LEAT ilikubali kuyaratibu vilidhoofisha kazi ya CAO. Zaidi ya hapo, kukubali kwa LEAT kwa hiari yao kuchochea ghasia kwenye machimbo kwa faida yao

kulisukuma CAO kuhusika na usalama wa watu walioshughulika katika jambo hili nje ya tume ya CAO. Usajili mbele ya CAO sio biashara ya mapato kwa njia ya ada na CAO inasikitishwa kujua kuwa LEAT ilidai malipo kutoka wenyeji kwa ajili ya huduma iliyotolewa na kampuni yao. CAO hugharimia gharama zote za uchunguzi na ingependa LEAT kupanga taratibu za ugavi wa tume ya uchunguzi, gharama ambazo zingeligharimiwa na CAO.

Kiambatanishi 1: Malalamiko

**LAWYERS' ENVIRONMENTAL ACTION TEAM (LEAT)**

*Mazingira, House, Mazingira Street, Mikocheni Area*
*P.O.BOX 12605,* Dar *es Salaam, Tanzania*
*Simu/Faksi: 255222780859*
*Barua pepe: leat@twiga.com*
***Mtandao:** http://www.leat.or.tz*

Kwa: Compliance Advisor/Ombudsman
2121 Pennsylvania Avenue, NW
Room F5K-292
Washington DC 20433
USA
Faksi: 202-522-7400
Barua pepe: cao-compliance@ifc.org

Sisi Lawyers' Environment Action Team (LEAT) tunatuma malalamiko rasmi juu ya Bulyanhulu Gold Mine Project. Malalamiko haya yameletwa kwa niaba yetu kwa niaba ya wateja wetu, jamii iliyopita ya wachimbaji wadogo wa migodi na wamiliki wa ardhi wa eneo la

Bulyanhulu chini ya Bulyahulu Small-Scale Gold Miners' Committee (walalamikaji wa Bulyanhulu). LEAT ni taasisi ya sauti ya wananchi juu ya sheria za mazingira ambazo ilikuwa ikizishughulikia pamoja na kwa niaba ya walalamikaji wa Bulyanhulu. Barua ya kuipa mamlaka LEAT kuwasililsha walalamikaji wa Bulyanhulu katika malalamiko haya kwa alama "A" na kuwa sehemu ya malalamiko.

LEAT na walalamikaji wa Bulyanhulu wanaweza kufikiwa kupitia anwani, namba ya simu na fax na barua pepe kama ifuatavyo:

Bw. Rugemeleza A.K. Nshala
The Lawyers' Environmental Action Team (LEAT)
Mazingira Hause, Mazingira Street
Mikocheni Area
PO Box 12605
Dar es Salaam
Tanzania.
Simu: (+255)22-278-0859
Faksi: (+255)22-278-0859
Barua Pepe: lissua@wri.org

NA

Bw. Tundu A. Lissu
Institutions and Governance Program
World Resources Institute
10 G Street, NE, Suite 800
Washington DC 20002
Simu: 202-729-7645
Faksi: 202-729-7759
Barua Pepe: lissu@wri.org

Msingi wa malalamiko ni kama ifuatavyo:

**Maelezo ya Mradi**

1. Bulyanhulu Gold Mine lipo katika eneo la Bulyanhulu wilaya ya Kahama, Mkoa wa Shinyanga ni mgodi mkubwa wa machimbo ya dhahabu ambao pia hutoa shaba na fedha.
2. Multilateral Investment Gurantee Agency (MIGA) inashiriki katika mradi kwa njia ya kutoa dhamana ya bima kisiasa yenye thamani ya Dora za Kimarekani 172 milioni iliyopitishwa Agosti 2000.
3. Mfadhili wa Mradi ni Kahama mining Corporation Limited ya Dar es Salaam, Tanzania ambayo iko katika ubiya kamili na Barrick Gold Corporation ya Toronto, Canada ( Mfadhili wa Mradi).

**Historia ya malalamiko**

a) Walalamikaji wa Bulyanhulu awali walikuwa wanaishi na kufanya kazi kama wachimba migodi wadogo, wafanya biashara wadogo, wakulima na wafanyakazi katika eneo linalojulikana kama Bulyanhulu katika wilaya ya Kahama, Mkoa wa

Shinyanga sehemu ya kati Magharibi ya Tanzania. Hata hivyo, Septemba 1994 wafadhili wa mradi waliwakilisha malalamiko juu ya eneo la Bulyanhulu kuhusiana na liseni iliyotolewa na Serikali ya Tanzania. Agosti, 1994 nakala ambayo imeambatanishwa na kuwekewa alama “B” na/ kuwa sehemu ya malalamiko haya.

b) Kutokana na liseni hii, wafadhili wa mradi walisababisha Ubalozi wa Kanada nchini Tanzania kuweka shinikizo la kisiasa kwa Serikali ya Tanzania kuwafukuza walalamikaji wa Bulyanhulu. (Walalamikaji wanarejea kwenye nyaraka zilizopatikana kutoka idala ya mambo ya nchi za Nje na Biashara ya Kimataifa (DFAIT) chini ya Canadian Access to Infomation ACT na kuwekewa“C” katika kudhibitisha malalamiko haya).

c) Wafadhili wa mradi pia walianzisha kesi mahakamani dhidi ya walalamikaji wa Bulyankulu katika Koti ya Mahakama Kuu Tanzania ili walalamikaji wa Bulyanhulu wafukuzwe kwa amri ya mahakama (Nakala za uamuzi na taratibu za Mahakama kuu ya Tanzania kwenye kesi hizi zimeunganishwa chini ya alama “D” na kuwa sehemu ya malalamiko haya.)

d) Kutokana na uamuzi mbaya uliofanywa na Mahakama Kuu ya Tanzania, wafadhili wa mradi waliomba rufaa kwenye Mahakama Kuu ya Rufaa Tanzania (Tanzania’s Highest Appellate court), lakini baadaye walifuta rufaa na kurudia hali ya kawaida kwa kutumia nguvu za kidiplomasia za dola kuwafukuza walalamikaji wa Bulyanhulu. (Nakala za maombi yaliyotumwa na wanasheria wa ‘wafadhili wa mradi” kwa Mahakama Kuu ya Rufaa Tanzania na mawasiliano ya maagizo ya Mwanasheria Mkuu yameambatanishwa na shauri hili na kuwekewa alama “F” na kuwa sehemu ya malalamiko haya). Walalamikaji wa Bulyanhulu wanarejea pia kwenye makala za sasa katika vyombo vya habari ambazo zimeambatanishwa katika ripoti hii na kuwekewa alama “F” kufanya kuwa sehemu ya malalamiko haya.

e) Julai 30, 1996 Serikali ya Tanzania ilitoa amri kwamba walalamikaji wa Bulyanhulu kuwa lazima waihame ardhi, makazi na mali yao katika masaa 24. Kikundi cha Polisi cha fanya fujo uone na vifaa vya kuporomolea mali ya wafadhili wa mradi vikiendeshwa na wafanyakazi vilipelekwa kwenye makazi na kijiji cha walalamikaji huko Bulyanhulu. Siku iliyofuata uhamishaji wa walalamikaji wa Bulyanhulu na ubomoaji wa makazi yao na uamishaji mali ulianza na kuendelea siku nyingi za Agosti1996. (Angalia kiambatanisho “C” na “F” na nakala za video zilizochukuliwa na wafadhili na polisi na Tanzania ambazo zimeambatanishwa na shauri hili na kupewa alama “G” na kuwa sehemu ya malalamiko.)

f) Katika kufanya hivyo, wafadhili wa mradi na serikali ya Tanzania walikwenda kinyume na amri ya mahakama kuu iliyounganishwa na shauri hili na kupewa alama “D”. Walalamikaji wa Bulyanhulu wanarejea pia kwenye matamko ya Serikali ya Tanzania kuhusiana na masuala yanayotiliwa mashaka yaliyoambatanishwa na shauri hili na kwa alama “H” na kufanyika sehemu ya malalamiko haya. Walalamikaji wa Bulyanhulu, kwa hurejea nyaraka zilizoandaliwa na au kwa ajili ya wafadhili wa mradi na kuwasilishwa kwa MIGA ambazo zimewekewa alama “I” katika kuthibitisha malalamiko haya.

g) Kwa hiyo, walalamikaji walilazimishwa kulihama eneo na sasa wanaishi katika kijiji cha Kakola, Kahama mjini, Mwamboka na maeneo ya mgodi ya Kezeria, katika Wilaya ya Kahama. Wale waliobaki katika eneo la Bulyanhulu ambapo kijiji cha Kakola ni sehemu wanaendelea kuishi kwa woga wa kuhamishwa kwa lazima na usiofidiwa kama mawasiliano yanavyoonyesha kati ya wafadhili wa mradi na Serikali ya Tanzania, nyaraka za mahakama zote zinaonyeshwa kwa alama "J" na kufanyika sehemu ya malalamiko haya.

**Malalamiko**

4. Walalamikaji wa Bulyanhulu wameonekana au wanaonekana wa kuathirika na athari za mradi kijamii na kimazingira kwa njia zifuatazo:

**Uhamisho wa Nguvu na ukosefu wa makazi wakati wafadhili wa mradi waliposhika hatamu kwenye eneo la mradi.**

a) Tunaamini kuwa makumi elfu ya walalamikaji wa Bulyanhulu walilazimishwa kuhama na kufukuzwa kwa nguvu kutoa eneo la Bulyanhulu wakati wafadhili wa mradi walipoingia katika ardhi, makazi na maeneo ya mgodi ya Bulyanhulu kwa nguvu na kinyume cha sheria kwa msaada wa nguvu za dola na Serikali ya Tanzania.
b) Tunaamini kwamba wafadhili wa mradi na serikali ya Tanzania walisusia na kushindwa kupanga, kugharimia na kutekeleza makazi mapya au mpango wa utoaji wa ardhi nyingine au makazi au msaada mwingine wa makazi kwa walalamikaji wa Bulyanhulu.
c) Tunaamini kuwa wafadhili wa mradi na Serikali ya Tanzania walishindwa na walikataa kulipa fidia iliyostahili, inayoridhisha, ya haki na haraka kwa ajili ya mali ya kilimo' mifugo na uharibifu wa makazi ikiwa ni pamoja mali ya biashara na ya nyumbani, upokonyaji wa haki ya mifugo, na uwekezaji wa vifaa vya machimbo, mashini, migodi ya madini, kipato kwa njia ya ajira na uendeshaji uchimbaji mdogo wa madini.

**Vitisho vya kufukuzwa na kuamishwa vinavyoendelea**

d) Tunaamini kwamba wafadhili wa mradi na Serikali ya Tanzania wameendelea kutumia vitisho au matumizi ya nguvu kuwafukuza na kuwahamisha idadi nyingine ya walalamikaji wa Bulyanhulu.
e) Tunaamini kwamba wafadhili wa mradi wa Serikali ya Tanzania wameendelea kukiuka na/au kuingilia vinginevyo furaha ya amani ya haki miliki ya walalamikaji wa Bulyanhulu ili kwa manufaa watumie ardhi yao kwa kilimo na mifugo; na kuwazuia kujenga nyumba za kuishi na biashara katika maeneo ya ardhi na makazi yao.
f) Tunaamini kuwa wafadhili wa mradi na serikali ya Tanzania wameshindwa na/au wamepuuzia kulipa fidia iliyostahili, inayotosheleza, za haki na haraka kwa ajili ya ukiukaji wa na /au kuingilia furaha ya amani ya haki miliki ya Bulyanhulu.

**Athari kwenye uchumi wa eneo la Bulyanhulu**

g) Tunaamini kuwa wafadhili wa mradi waliharibu uchumi wa asili wa eneo la Bulyanhulu na hata zaidi ya hapo, kuangamiza watu katika eneo la Bulyanhulu, faragua walalamikaji wa Bulyanhulu kama matokeo ya utaifishaji wa ardhi ya kilimo na ufugaji, uharibifu wa mali ya biashara ya makazi, uponyokaji wa uwekezaji katika machimbo ya migodi, mashini na nyenzo za kazi na upotezaji wa nafasi za ajira.
h) Tunaamini kuwa wafadhili wa mradi walishindwa kutoa makazi sawa na yale au mazuri zaidi; vianzio vya maisha vizuri au vya kulingana na vile vya zamani katika uwanja wa uchumi na nafasi za ajira kwa walalamikaji waliosalia katika Bulyanhulu.
i) Tunaamini kwamba wafadhili wa mradi wa uwekezaji hawakuhusika na juhudi za upunguzaji wa umaskini nchini kwa kushindwa kuchangia kwa njia ya haki na sahihi kwenye mapato ya serikali katika nyanja ya ushuru mrabaha na malipo mengine.
j) Tunaaini kuwa uharibifu wa nafasi za ajira ambazo zilikuwa zinapatikana kabla kabla ya maombi ya kibali cha eneo la Bulyanhulu, wafadhili wameshindwa kubuni nafasi za ajira zenye maana au kama zilezile na kwa hiyo kukwamisha malengo ya taifa katika kuondoa umaskini.

**Kushindwa kwa wafadhili wa mradi kutimiza sheria ya Tanzania katika kuchukua eneo la mradi la Bulyanhulu**

k) Tunaamini kwamba wafadhili wa mradi walishindwa na/au kupuuzia kibali ambacho kwa hakika na sahili kilielezea eneo la milki;
l) Tunaamini kwamba wafadhili wa mradi na Serikali ya Tanzania walishindwa na /au walipuuzia kufuata taratibu zifaazo au kuingilia haki miliki ya walalamikaji wa Bulyanhulu;
m) Tunaamini kuwa baada ya kuamua kuwapeleka walalamikaji wa Bulyanhulu kwenye Mahakama ya Tanzania, wafadhili wa mradi walishindwa na/au walipuuzia kutii maagizo ya sheria na maamuzi ya Mahakama ya Tanzania;
n) Tunaamini kuwa wafadhili wa mradi kadhalika walitimiza vitendo au walishindwa na/au kupuuzia kutumiza matendo yaliyolalamikiwa kama ilivyotajwa kwenye haya A-F.

**Uchunguzi wa athari za mazingira na jamii haukuwa sahihi na haukukamilika**

o) Tunaamini kuwa wafadhili wa mradi walishindwa na/au walipuuzia kuufanya uchunguzi wa athari ili na kuzishughulikia kabla ya kuingia kwao na kuomba kibali cha eneo la Bulyanhulu na kabla ya kuhamishwa na kufukuzwa kwa walalamikaji wa Bulyanhulu;
p) Tunaamini kwamba wafadhili wa mradi walishindwa na/au walipuuzia kufanya mashauriano kamili na ya manufaa na walalamikaji wa Bulyanhulu kabla hawajaingia na kumiliki eneo la Bulyanhulu.
q) Tunaamini kuwa wafadhili wa mradi walitoa, walifadhili, walichapisha na kuwasilisha kwa MIGA, Serikali ya Tanzania na kwa raia uchunguzi wa athari za mazingira, mpango wa kuthibiti mazingira na mpango wa maendeleo ya jamii ambao haukuandaliwa sawasawa; wenye makosa, wa uongo na wenye habari

inayopotosha na maamuzi kuhusu kibali, mali na huendeshaji wa Bulyanhulu Gold Mine.

r) Tunaamini kwamba baada ya kuamua kubadili uchunguzi yakinifu kwenye mpango wa utekelezaji wa mradi, wafadhili wa mradi walishindwa kuandaa, kuchapisha na/au kuwasilisha kwa MIGA Serikali ya Tanzania na kwa raia nyongeza yoyote ya taarifa juu ya makadirio ya athari za mazingira na/au mipango ya udhibiti wa mazingira kuhusu mabadiliko ya uchunguzi yakinifu kwenye mpango na/au utekelezaji wa mradi ambao ungelikuwa na athari wazi katika mazingira kwa walalamikaji wa Bulyanhulu.

**Ufichaji wa habari**

s) Tunaamini kuwa wafadhili wa mradi walishindwa kuandaa na/au kutoa kwa MIGA, Serikali ya Tanzania na kwa raia kumbukumbu zote zenye habari kama taifa na hali halisi juu ya kibali, mali na uendeshaji wa Bulyanhulu Gold Mine pamoja na matendo na mambo yaliyoachwa mengi katika haya zilizoendelea.

t) Tunaamini kwamba wafadhili wa mradi walishindwa kutoa wazi taarifa juu ya athari za mazingira, mpango wa uthibiti wa mazingira na mpango wa maendeleo ya jamii iliyowasilishwa kwa MIGA, Serikali ya Tanzania na kwa raia juu ya madai nyeti yaliyoendelea juu ya ukatili wa haki za binadamu vilivyofanywa na wafadhili wa mradi na Serikali ya Tanzania juu ya hali ya kibali cha wafadhili wa mradi, mali na uendeshaji wa mradi.

u) Tunaamini kuwa wafadhili wa mradi walishindwa na/au kupuuzia kutoa wazi na/au kukubali katika taarifa ya athari za mazingira, mpango wa uthibiti wa mazingira, na mpango wa maendeleo ya jamii kuhusu taarifa au habari iliyokuwepo kuhusu ukiukaji wa malalamiko ya ukiukaji wa haki za binadamu dhidi ya walalamikaji wa Bulyanhulu ambao ulitendeka hata wafadhili wa mradi na Serikali ya Tanzania pasipo kujua.

v) Tunaamini kwamba wafadhili wa mradi walishindwa na /au walipuuzia kutoa kwa MIGA, Serikali ya Tanzania na raia taarifa za nyongeza juu ya athari za mazingira na/au mpango wa kuthibiti mazingira, kama ulikuwepo, juu ya mabadiliko ya uyakinifu na/au utekelezaji wa mradi ambao ungelikuwa na athari wazi za mazingira kwa walalamikaji wa Bulyanhulu.

**Upungufu wa MIGA kuhusu uangalifu wa uchunguzi**

w) Tunaamini kuwa MIGA ilishindwa kufanya uchunguzi yakini na wa ustadi kuusiana na ukweli na hali halisi juu ya kibali cha wafadhili, mali na uendeshaji wa Bulyanhulu Gold Mine ili kutokeza ukweli wa taarifa iliyowasilishwa na ukweli wa maamuzi yaliyofikiwa na wafadhili wa mradi kabla kufanya uamuzi kutoa dhamana ya ulinzi wa kisiasa kuhusiana na mradi.

**Ukiukaji wa MIGA juu ya sera yake ya utoaji wa habari**

x) Tunaamini kuwa MIGA ilisajili au kuandaa na/au kufunua wazi kwa walalamikaji na washika dao wengine kumbukumbu zote za taarifa kuhusu ukweli na hali halisi

kuhusu kibali cha wafadhili wa mradi, mali na uendeshaji wa mradi bila kujali maombi ya mara kwa mara kutoka kwa walalamikaji na washika dao wengine kufanya hivyo.

**Hatua zilizochukuliwa na walalamikaji**

5. Hatua zifuatazo zilichukuliwa nasi kwa kujaribu kutatua tatizo:
    a) Tumeandika mara mbili kwa Mheshimiwa Rais Benjamini William Mkapa, Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa mara zote mbili tumemuomba yeye na serikali yake kujitokeza katika masuala haya na kumaliza lolote au makosa yote ambayo yatakuwa yametendeka dhidi ya jamii za Bulyanhulu, kadhalika kuhakikisha kuwa ukiukaji wa sheria za Tanzania umechunguzwa kwa kina, na inapobidi na kulazimika, kuadhibu kwa mujibu wa sheria za Tanzania. Nakala za barua zimeambatanishwa na kuwekwa alama “K” na kufanya kuwa sehemu ya malalamiko haya.
    b) Tumeandika mara mbili kwa Mkurugenzi wa idara ya uchunguzaji wa kesi za jinai katika jeshi la polisi la Tanzania tukieleza makosa yaliyoorodheshwa hapa na kumuomba kuangalia kuwa makosa hayo yanachunguzwa kwa kina, na inapobidi ya kulazimika, kuadhibu kulingana na sheria za Tanzania. Tutarejea kwa mawasiliano haya yaliwekewa “L” katika kuthibitisha malalamiko haya.
    c) Mara mbili tumeandika kwa MIGA na mara moja kwa Canada’s Export Devolopment Corporation (“EDC”) tukiziomba taasisi hizi mbili kushughulikia jambo hili na kuangalia kama mojawapo na/au makosa yote yanachunguzwa kwa uhuru, na inapobidi na kulazimu, kosa lolote lisahihishwe kwa mujibu wa sera za MIGA na sheria zinazoongoza EDC. Barua hizi zimeambatanishwa katika shauri hili kwa alama “M” na kufanyika sehemu ya malalamiko haya.
    d) Tumewaandikia wafadhili wa mradi tukiwaomba kupatiwa nakala hususani, ripoti na ushahidi juu ya mali ya wafadhili wa mradi. Angalia barua kwa wafadhili wa mradi imeambatanishwa katika shauri hili na kuwekewa alama “N” kufanya sehemu ya malalamiko haya.
    e) Tumekutana na kuwa na mazungumzo pamoja na maofisa wa MIGA, Benki ya Dunia, EDC; wafadhili wa mradi pamoja na maofisa wa Serikali ya Tanzania, Kanada, Marekani, Uingereza na Uholanzi waliochaguliwa au kuteuliwa kuhusiana na maswala haya.

**Hatia zilizochukuliwa na wafadhili wa mradi, MIGA na Serikali ya Tanzania**

6. Hatua zifuatazo zilichukuliwa na wafadhili wa mradi, MIGA na serikali ya Tanzania kwa kuitikia hatua za walalamikaji:

    **Wafadhili wa mradi**

    a) Wafadhili wa mradi wameitikia kwa kuyakana madai yote ya matendo mabaya yaliyowahusu.
    b) Wafadhili wa mradi wamechukua hatua kusawazisha maeneo yote ambazo yanadaiwa kuwepo ukiukaji wa haki za binadamu jambo linaloonekana kuwa ni

majaribio ya kuharibu kila ushahidi wa matendo mabaya yanayohusu upande wao.

c) Wafadhili wa mradi wamebuni uongo na / au hatari na inayopotosha kwa uchunguzi huru na maamuzi kutokana na madai ya ukiukaji wa haki za binadamu. Tutarejea kwenye barua na nyaraka nyingine kutoka wafadhili wa mradi kuhusu masuala ambayo yameambatanishwa kwenye shauri hili kujulikana kwa alama “O” na kuwa sehemu ya malalamiko haya.

**MIGA**

d) Miga pia waliitikia kwa kuzilinda vikali hatua za wafadhili wa mradi na kuendesha na kukana madai yote juu ya matendo mabaya kwa upande wao na ule wa wafadhili wa mradi.

e) MIGA ilibuni uongo na/au habari ya kupotosha juu ya uchunguzi na maamuzi kutokana na yale yaliyohusu madai ya ukiukaji haki za binadamu. Tutarejea kwenye barua na nyaraka za mradi kutoka MIGA ambazo zimeambatanishwa kwenye shauri hili na kujulikana kwa alama “P” na kuwa sehemu ya malalamiko.

**Serikali ya Tanzania**

f) Serikali ya Tanzania imeitikia kwa kuyakana madai yote yanavyowahusu wenyewe na tabia ya wafadhili wa mradi kuhusu kibali, mali na uendeshaji wa Bulyanhulu Gold Mine.

g) Serikali ya Tanzania imeitikia kwa kutokeza uongo; taarifa yenye kupotosha au utata juu ya uchunguzi wake kwa madai ya ukiukaji wa haki za binadamu. Tutarejea kwenye matamko rasmi kutoka serikali ya Tanzania ambayo yameambatanishwa na kupewa alama “O” na kufanya sehemu ya malalamiko hayo.

h) Serikali ya Tanzania imechukua hatua kuwabughudhi, kuwaogopesha, na/au kwatisha walalamikaji na kila mtu au watu waliojaribu kuchunguza au kuuliza ukweli na hali halisi kuhasiana na kipato cha wafadhili wa mradi, mali na uendeshaji wa eneo la mgodi la Bulyanhulu. Vitendo vya serikali vikiusisha polisi, upolaji, na upekuzi wa ofisi za LEAT na nyumba za maofisa wa LEAT, kukamatwa na kuwekwa rumande maofisa wa LEAT na wahakiki wengine wa serikali waliokuwa na hati ya kuwafukuza Bulyanhulu na madai ya ukiukaji wa haki za binadamu; na vitisho vya kuanzisha kesi za uhaini dhidi ya walalamikaji na watu wengine waliojaribu kuchunguza na/au kuuliza wale waliohusika serikali na vibali vya kuamisha na ya haki za binadamu. Tutarejea taarifa za sasa za vyombo vya habari ambavyo viko katika alama “R” ili kudhibitisha malalamiko haya.

7. Majina ya watu ya kuwasiliana nao katika MIGANI
   a) Bw. Gerald T. West
   b) Bw. Marcus Williams
   c) Bi. Moina Varkie

8. Ifuatayo ni utondoti wa sera, mwongozo na taratibu za MIGA ambazo kwazo tunaamini hazikufuatwa:
    a) Makazi mapya yasiyotegemewa: kusudi mradi huu uweze kuendelea, mamia elfu ya watu ilibidi kuamishwa. Hili lilifanyika kwa kutumia nguvu pasipo mpango wa makazi mapya. Makazi mapya yasiyotegemewa bado yanaendelea pasipo mpango wowote wa makazi mapya.
    b) Sera ya uchunguzi wa mazingira: shughuli za uchunguzi wa athari kwa mazingira ziliendelea baada ya uamishaji wa lazima na ufukuzaji wa walalamikaji wa Bulyanhulu; na hivyo walishindwa kuyafikilia shughuli na maslahi yao.
    c) Kushauriana na wananchi: Mashauriano na wananchi yalifanyika baada ya walalamikaji wa Bulyanhulu kuwa wamehamishwa kwa nguvu. Pia mashauriano yalifanyika tu kwa idara na wateuzi warasimu wa serikali pasipokuwepo ushirikishwaji wa taasisi zisizo za kiserikali za mkoa au kitaifa.
    d) Sera ya ulinzi kijamii: Hakuna ulinzi wowote wa jamii uliofanyika kushughulikia athari za kijamii na kiuchumi juu ya uhamisho wa nguvu kwa walalamikaji wa Bulyanhulu, wala hakuna ulinzi wowote uliochukuliwa kupunguza athari mbaya za kijamii na kiuchumi zinazoendelea ambazo husababishwa na mradi kwa jamii jirani.
    e) Utoaji wa sera ya habari: MIGA wakati wote imekatalia maombi ya kutoa kwa wananchi habari au kumbukumbu yoyote iliyokuwa imekusanywa katika uchunguzi wake wa yakini na kuwa huo ulitegemea katika kutoa maamuzi juu ya utoaji wa dhamana ya bima ya kisiasa kwa ajili ya mradi.
    f) Kipengele 12 (d) cha sheria ya MIGA kinachosema kuwa: katika kudhamini kitega uchumi, shirika lazima lithibitishe mpango timamu wa uchumi wa kitega uchumi na mchango wake wa maendeleo ya nchi.
    g) Kifungu cha 12 (d) cha sheria ya MIGA vilevile husema kuwa katika kudhamini kitega uchumi, shirika lazima lithibitishe “kukubaliana na sheria na taratibu za uwekezaji katika nchi hiyo.”

9. Tungependa kuona tatizo hili lina tatuliwa kama ifuatavyo:

    a) Fidia kamili, ya haki na kamili inalipwa kwa walalamikaji wa Bulyanhulu waliohamishwa pasipo kutegemea na pasipo mpango wowote wa makazi.
    b) Fidia kamili, ya haki na ya kurithisha lazima ilipwe kwa walalamikaji wote wa Bulyanhulu ambao ardhi yao ya kilimo na mifugo ilipokonywa; mali na makazi, biashara na nyumba kubomolewa; uwekezaji katika machimbo ya madini kupokonywa, madini na zana za kazi kufukiwa; na nafasi za ajila kupotea.
    c) Faida kamili, ya haki na ya kuridhisha lazima ilipwe kwa walalamikaji waliobaki wa Bulyanhulu ambao haki yao ya milki inaendelea kukiukwa na/au inaingiliwa na matendo ya wafadhili wa mradi. Kadhalika, wafadhili wa mradi waache vitendo vya sasa au vitakavyokuwepo baadaye ambavyo vinaingilia au kukiuka furaha ya walalamikaji na Bulyanhulu juu ya haki miliki yao.
    d) CAO inapashwa kuchunguza kwa upya utaratibu halisi wa MIGA juu ya uchunguzi yakini wa sasa ili kuchunguza kama MIGA imechukua hatua muhimu kuhakikisha kuwa mradi umezingatia sera za MIGA kabla haijatoa dhamana ya bima wa kisasa kwa Bulyanhulu Gold Mine.

e) CAO lazima ichunguze upya taarifa za athari za mazingira na jamii ambazo wafadhili wa mradi waliziwakilisha kwa MIGA na kulinganisha na taarifa zilizopo katika malalamiko haya ili kutokeza taarifa kamili na kweli za athari za mazingira na jamii na ukweli wa maamuzi yaliyofanyika juu ya taarifa za mazingira zilizowasilishwa kwa MIGA na Serikali ya Tanzania.
f) CAO lazima ichunguze vitisho vinavyoendelea vya ufukuzwaji na uamishwaji, na athari mbaya za jamii na uchumi zisababishwazo na mradi wa madini wa Bulyanhulu kwa jamii jirani.
g) CAO lazima ichunguze kama MIGA imetii sera zake juu ya ulinzi hasa katika sera ya makazi yasiyotazamiwa, pia ichunguze kama au kwa jinsi gani ufadhili wa fedha wa MIGA unaendeleza malengo yake katika utokomezaji wa umasikini.
h) CAO lazima ichunguze upya utiifu wa MIGA katika sera yake ya utoaji wa taarifa katika kuitikia maombi kwa ajili ya taarifa kulingana na mradi huu na lazima iagize MIGA utoaji kamili wa kumbukumbu zote zinalindwa na vipengele vya siri hili kuruhusu ushirikishwaji wa wananchi katika kutatua malalamiko haya.
i) CAO lazima itoe wito wa kuanzisha tume huru ya uchunguzi inayokubaliwa na walalamikaji wa Bulyanhulu kadhalika wafadhili wa mradi na Serikali ya Tanzania kuchunguza kwa uhuru, uwazi wa kina ukweli na hali halisi juu ya kibali, mali na uendeshaji wa mradi, na inapolazimu na kustahili, ifanye mapendekezo ya maamuzi ya malalamiko haya.
j) CAO lazima ichunguze kama MIGA imetekeleza ipasavyo kuhusu uchunguzi yakini kabla ya kupitisha dhamana kuhusiana na faida za kiuchumi na kijamii zitakazopatikana kwa jamii za pale katika eneo Bulyanhulu na sera za Tanzania juu ya nafasi za ajira, mapato kutokana na ushuru, mrabaha na malipo mengine. Nyongeza, CAO lazima ichunguze kama MIGA ilifikilia katika uchunguzi yakini namna nyingine inayowezekana kwa mradi ambayo ingetokeza faida zaidi au zenye kumithilisha za kijamii na kisiasa, lakini zenye athari mbaya pungufu.

Tunakumbuka kwamba Barrick Gold Corporation, kampuni kanzu ya sasa ya wafadhili wa mradi, na MIGA haikuingia moja kwa moja katika mradi mpaka kipupwe 1999 wakati wa matukio yote yanayoyalalamikiwa yalikuwa yametokea. Hata hivyo, tunaamini kwamba kuna uhusiano wa moja kwa moja na matukio kabla ya 1999 na ya sasa kuhusiana uendeshaji unaofanywa na wafadhili wa mradi katika eneo la Bulyanhulu. Kuna uhusiano wa moja kwa moja kwa sababu matukio hayo yalikuwa masharti ya awali kwa ajili maendeleo ya uendeshaji wa sasa kwa wafadhili wa mradi. Mradi usingelisonga mbele pasipo kuanza kushughulikia maswala ya mamia elfu ya watu ambao waliishi na kufanya kazi katika eneo linalolalamikiwa.

Tunaamini kwamba upo uhusiano wa moja kwa moja hata kama muda uliopita kati ya matukio yanayolalamikiwa kwa upande mmoja, na pia kunakujiingiza kwa MIGA kwa upande mwingine. Uhusiano huu wa moja kwa moja unaendelea hata kama kuna mabadiliko ya muundo wa umilikaji wa wafadhili wa mradi kwa maana wamilikaji wa sasa wa mradi na MIGA wamefaidika, wananufaika na wamekuwa wakinufaika kimapato kutokana na matukio kabla ya 1999 ambayo yanalalamikiwa. Kwa kweli, tunajua kuwa mabadiliko katika muundo wa umilikaji haukubadilisha nafsi au utambulisho kisheria wa wafadhili wa mradi.

Kwa hiyo tunaamini kuwa hali halisi kuhusu matukio kabla ya 1999 hupatana na maana ya msingi ya eneo la mradi. Kwa hiyo, matukio haya katika eneo la uchunguzi yakini ungelikuwa

umefanyika na wafadhili wa mradi na MIGA. Ni matumaini yetu kwamba CAO watakubaliana nasi kwamba madai ya uchunguzi yakini wa MIGA wakati wa maandalizi ya mradi lazima yatumike kwenye matukio yanayotangulia kujiingiza kwao katika mradi tajwa kama mradi kama matukio hayo yalikuwa na maana kwa maendeleo ya mradi. Ni muhimu kwamba Kundi la Benki ya Dunia halikutuma ujumbe kwa mambo wazi ambayo hayakustahili katika maandalizi ndipo mradi ukubaliwe hata kama yalitokea kabla ya kujiingiza moja kwa moja kwa MIGA au [yalikuwa] chini ya umilikaji wa mali mbali na wafadhili wa sasa wa mradi.

10. Tumewasiliana wa watu wafuatao katika kujaribu kutatua masuala haya:
    - h) Bw. James Wolfensohn, Rais wa MIGA na Kundi la Benki ya Dunia.
    - i) Bw. Motomichi Ikawa, Makamu wa Rais Mtendaji wa MIGA
    - j) Bw. Patrick J. Garver, Makamu wa Rais Mtendaji na Mshauri Mkuu, Barrick Gold Corporation.
    - k) Bw. Pieter Stek, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Dunia akiwakilisha Uholanzi.
    - l) Bw. David Herscovitch wa Shirika la Maendeleo la Biasharanje la Kanada.
    - m) Bi. Jennifer Rosebrugh wa Idara ya Mambo ya Nchi za Nje na Bishara ya Kimataifa wa Serikali ya Kanada.
    - n) Bw. Paul Stothart wa Ofisi ya Waziri wa Biashara ya Kimataifa wa Serikali ya Kanada.
    - o) Bw. Jeffrey McLaren wa Ubalozi wa Kanada Nchini Tanzania.
    - p) Mheshimiwa Alexa McDonough, Kiongozi wa National Democratic Party Katika Bunge la Wananchi la Kanada.
    - q) Mheshimiwa Lincoln Clifford, Mbunge katika Bunge la Wananchi la Kanada.
    - r) Mheshimiwa Pierre Paquette, Mbunge katika Bunge la Wananchi la Kanada.
    - s) Bw. William Price wa Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Serikali ya Uingereza
    - t) Hon. Cynthia Mckinney wa Bunge la Marekani.
    - u) Bw. Hein Copper wa Tasisi za Fedha Idara ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Serikali ya Uingereza.

11. Maelezo muhimu yaungao mkono malalamiko haya ni kama ifuatavyo:
    - a. Kumbukumbu za mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa ya Tanzania kuhusiana na kesi za mahakamani zilizoanzishwa na/au kuhusisha wafadhili wa mradi na baadhi ya kibali na milki ya wafadhili wa mradi wa Bulyanhulu Gold Mine.
    - b. Barua za kiofisi kati ya walalamikaji wa Bulyanhulu, maofisa wa Serikali ya Tanzania na wafadhili wa mradi kabla ya kibali na milki ya wafadhili wa mradi wa Bulyanhulu Gold Mine.
    - c. Taarifa za magazetini kuhusiana na maelezo na hali halisi kuhusiana na kibali na milki ya wafadhili wa mradi na uendeshaji wa mradi wa Bulyanhulu Gold Mine hasa juu ya malalamiko ya walalamikaji wa Bulyanhulu.
    - d. Nyaraka za mradi na taarifa ya mazingira katika mtindo wa taarifa za athari za mazingira, mpango wa udhibiti wa mazingira na mpango wa maendeleo ya jamii ulioagizwa, andaliwa na kuchapishwa na wafadhili wa mradi na kuwasilishwa kwa MIGA na Serikali ya Tanzania.
    - e. Taarifa zilizoandaliwa na kuchapishwa na wafadhili wa mradi kuhusu kibali, milki na uendeshaji wa Bulyanhulu Gold Mine.

Tarehe 14 Januari 2002

Imetiwa sahihi

Kiambatanishi 2

**<u>LAWYERS' ENVIRONMENTAL ACTION TEAM</u>**
**<u>(LEAT)</u>**

*Mazingira, House, Mazingira Street, Mikocheni Area*
*P.O.Box 12605,* Dar *es Salaam, Tanzania*
*Simu/Faksi: 255 22 2780859*
*Barua pepe: leat@twiga.com*
*Mtandao: http://www.leat.or.tz*

Februari 11, 2002

Kwa: Compliance Advisor/Ombudsman
2121 Pennsylvania Avenue, NW
Room F5K-292
Washington DC 20433
USA
Faksi: 202-522-7400
Barua pepe: cao-compliance@ifc.org

**YAH: NYONGEZA YA TAARIFA KUHUSU MALALAMIKO DHIDI YA BULYANHULU GOLD MINE**

Kwa kufuatilia malalamiko yaliyosajiliwa Januari 15, 2002, LEAT na walalamikaji wa Bulyanhulu hapa tunawasilisha nyongeza ya taarifa katika uungaji mkono madai kwamba wafadhili wa mradi hawakutimiza sheria za Tanzania, na hivyo kukiuka nyongeza za kipengele cha 12(d) cha mapatano ya MIGA chenye kudhibitisha utekelezaji wa mradi kulingana na sheria na taratibu za uwekezaji kwenye nchi husika

1. Madondoo kutoka Sheria ya Madini ya Tanzania 1979, Sheria namba 17 ya 1979 ambayo kwayo madhumuni ya leseni ya uchimbaji madini katika eneo la Bulyanhulu ilitolewa. Kwa ustahifu walalamikaji wanavuta nadhari kwa CAO katika nyongeza sheria zifuatazo ambazo ni muhimu sana kwa mlalamikaji, na ambazo hazikutekelezwa na mfadhili wa mradi.

    a. Fungu 31 (1)(c) hudai leseni yoyote ya uchimbaji madini inayotolewa "kuwa na maelezo na mpango juu ya eneo la ardhi (lililokuwa) linalotolewa..." Inatarajiwa kwamba kulingana na "maelezo na mpango wa eneo" linalozungumziwa hapa, kulihitajika maelezo na mpango sahihi wa eneo hili linalohusika, na kwamba leseni ya uchimbaji haikueleza kwa usahihi eneo hilo la ardhi au ilitoa mpango mbaya; kwa hiyo liseni hiyo haiwezi kuwa halali kulingana na makusudi ya kifungu hiki.

    b. Fungu 31(2) (b) husisitiza wajibu kwa wafadhili wa kuambatanisha leseni za uchimbaji wa madini juu ya ".... maelezo ya mapendekezo ya leseni kwa ajili ya ajira na uelimishaji wa raia wa Tanzania.

    c. Fungu 48 husisitiza "sheria muhimu za utumiaji haki" za wamilikaji wa mgodi kulingana na haki za wamilikaji wa ardhi ambao ardhi zao zinaathirika na leseni. Sheria zilizuia

wafadhili wa mradi kutokuingia kwenye eneo la Bulyanhulu pasipo kibali kilichoandikwa cha walalamikaji wa Bulyanhulu.

d. Fungu 81(1) uhusika na “fidia kwa usumbufu wa haki “n.k. Fungu husomeka: “Wakati wa kipindi cha upelelezi, uchimbaji au endeshaje mgodi unaosababisha kila aina ya usumbufu wa haki za mmilikaji kisheria wa ardhi au uharibifu wowote kuhusu mazao, miti, majengo, akiba au kazi, mmilikaji halali wa mgodi aliyesajiliwa au mmilikaji mwenye haki ya uchimbaji wa madin... anapaswa kulipa kwa mmilikaji halali fidia inayostahili na inayofaa kutokana na usumbufu au uharibifu kwa mujibu wa haki au maslahi .... ya mmilikaji halali kwenye mali inayohusika”

2. Nakala za sheria mbalimbali zilizotangazwa chini ya fungu la 69 la Sheria ya Madini ya 1979 inayotunuku mamlaka ya Waziri wa Madini kutenga maeneo ya madini kwa ajili ya kampuni pekee ya uchimbaji wa madini na mgodi kwa mtaalamu mzawa. Chini ya fungu 96(1), “Waziri akiona kuwa kutakuwepo maslahi ya uma akihimiza uchimbaji wa mgodi wa madini kwa eneo lolote la ardhi ikiwa njia zitakazotumika hazidai matumizi makubwa au teknologia maalumu ... anaweza kutenga eneo hilo... na kudhiilisha aina ya madini katika eneo hilo.” Uteuzi na udhiilishaji lazima ufanyike kwa njia ya tangazo litakalochapishwa katika Gazeti la Serikali. Sheria pia inaweza kuzuia eneo lolote lililotengwa kupewa wachimbaji wakubwa au uendeshaji wa mgodi na mashirika sawa na wafadhili hawa wa mradi.

a. Tangazo la mgodi (katika eneo lilitengwa) lilitangazwa rasmi na Waziri wa wakati huo wa Maji, Nishati na Madini Al-Noor Kassum, na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali la Januari 18, 1980 kama tangazo la Serikali namba 6 la 1980. Tangazo, pamoja na mambo mengine, lilitenga maeneo mazima ya katika mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Mara, Singida, Tabora, Mbeya na Rukwa, ambapo uchimbaji wa madini na mgodi wa dhahabu ungelifanyika kwa “njia ya ambazo hazitaingiza matumizi makubwa au teknologia maalumu.”

b. Marekebisho ya tangazo la madini (maeneo yaliyotengwa) lilitangazwa rasmi mwaka1982 na Waziri wa wakati huo wa Maji, Nishati na Madini Jackson Makweta, na kutangazwa katika Gazeti la Serikali la Desemba 17, 1982 kama tangazo la Serikali namba 54 la 1982. Tangazo liliondoa mikoa ya Shinyanga na Mwanza kutoka maeneo yaliyotengwa na kutangazwa katika Tangazo la 1980 yakawa maeneo ya wachimbaji madini maalumu ya dhahabu.

c. Marekebisho ya Tangazo la Madini (maeneo yaliyotengwa) la mwaka 1983 lililotangazwa na Waziri wa wakati ule wa Madini, Paul Bomani, na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la Januari 6,1984 kama Tangazo la Serikali namba 2 la 1984. Tangazo hilo sio kwamba lilirudisha tu mikoa ya Shinyanga na Mwanza katika kundi “maeneo yaliyotengwa,” lakini pia liliongeza mikoa ya Iringa, Kagera na Kigoma.

d. Marekebisho ya Tangazo la Madini (katika maeneo yaliyotengwa),mwaka 1984, lilitangazwa na Waziri wa wakati huo Al-Noor Kassum na kuchapishwa mnamo Februari 1,1985 kama tangazo la Serikali namba 34 la mwaka 1984. Tangazo hili lililorekebishwa na Tangazo la Serikali 2 la mwaka 1985 ambapo km.417 za mraba katika eneo la

Rwamagaza; km.1035 za mraba katika eneo la Geita; 2500 za mraba katika eneo la Musoma; km. 2403 za mraba katika eneo la Iramba – Sekenke; na km.605 za mraba katika maeneo ya Kaskazini na Mashariki mwa Mara, haya yote yalitolewa katika maeneo yaliyotengwa ya migodi ya dhahabu. Eneo la Bulyanhulu hali kuathiriwa na marekebisho, maana yake lilibaki kuwa chini ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya "uchimbaji na mgodi (wa dhahabu) kwa njia zisizohitaji matumizi makubwa au teknologia maalumu.

e. Tangazo la Madini (katika maneno yaliyotengwa) la 1987, lilitangazwa Julai 22, 1988 kama Tangazo la Serikali namba 230 la 1987. Ijapokuwa Tangazo hili lilibatilisha Tangazo la 1983, badiliko kuu lililofanyika lilihusu Mkoa wa Kigoma, eneo lililotengwa katika tangazo hili, liliondolewa kutoka kundi hili wakati Mkoa wa Morogoro uliongezwa katika orodha ya maeneo yaliyotengwa. Mikoa ya Shinyanga na Mwanza na hivyo eneo la Bulyanhulu – ilibaki kama eneo lililotengwa.

f. (Marekebisho) ya Tangazo la Madini (Kwenye maeneo yaliyotengwa) mwaka 1996 lilitangazwa rasmi na Waziri wa wakati huo wa Nishati na Madini, William Shija na lilichapishwa Juni 14, 1996 kama Tangazo la Serikali namba 106 la 1996. Ingawa haikuelezwa sawasawa sababu ya kutolewa, Tangazo hili lilihusu kurekebisha Tangazo la 1985 kwa kurudisha kwa upya sehemu kubwa ya maeneo la Kaskazini na Mashariki mwa Mara katika hali yake ya kuwa chini ya "maeneo yaliyotengwa." Kadhalika, eneo la Bulyanhulu lilibaki kuwa eneo lilitengwa kulingana fungu la 69.

Historia hii ya Sheria huonyesha wazi kuwa kipindi ambacho Bulyanhulu ilitengwa kisheria kwa ajili ya mashirika kama ya wafadhili hawa wa mradi na kwa waendeshaji wakubwa wa mgodi kilikuwa Desemba 18,1982 hadi Oktoba 12, 1983 wakati mikoa ya Shinyanga na Mwanza ilipokuwa haipo chini ya maeneo yaliyotengwa. Jumlisho la msingi linaloweza kujifikiwa katika uchambuzi huu, na kutokana na makusudi ya leseni uchimbaji iliyotolewa kwa KMCL kuhusu eneo la Bulyanhulu, kulitendeka kwa njia ya uvunjaji sheria wa fungu la 69 la Sheria ya madini ya Tanzania ya 1979 na nyongeza ya sheria zilizoorodheshwa chini yake. MIGA ilipewa – wakati wa uchunguzi yakini –kuhakikisha wafadhili wa mradi wanatimiza nyongeza hizi za sheria ya Tanzania, kwa mujibu wa sera zake za hifadhi. Ni imani yetu kwamba MIGA ilipuuza na/au ilishindwa kutimiza wajibu huu.

Tarehe 11 Februari, 2002

Imetiwa sahihi na Tundu A.M. Lissu
(Kwa niaba ya Walalamikaji )